# Kristo 10



Published by the Comic Bible Society, LLC
Copyright © 2021

Kingstone Comics maintains copyright to this comic book as provided by United States copyright law.

Print and digital copies of this version may be freely distributed without penalty under a Creative Commons license.




MATHAYO 21:18-19; MARKO 11:12-14






MATHAYO 21:12; MARKO 11:15; YOHANA 19:45




MATHAYO 21:13-14; MARKO 11:16-17; LUKA 19:46; ISAIYAH 56:7; YEREMIAH 7:11






MATHAYO 21:15-16; MARKO 11:18; LUKA 19:47-48; ZABURI 8:2


WAWEZA KUMUAMINI MTU HUYU NIKODEMU?
VITU ANAVYOSEMA?
NDIO...SIO KAMA MTU YEYOTE NIMEWAHI KUKUTANA NAYE...
MIAKA TATU KABLA. SHEREHE YA PASAKA.
...SKIZA NISEMAPO, HAKUNA AWEZAYE KUUONA UFALME WA MUNGU KAMA HAJAZALIWA KWA MARA YA PILI.
HIYO INA MAANA GANI? HAIWEZEKANI!
MWILI WAZAA MWILI.
LAKINI ROHO YAZAA ROHO.
LAKINI KIVIPI?
UNAWAFUNZA WAISRAELI LAKINI HUELEWI?
VILE AMBAVYO MUSA ALIMUINUA NYOKA JANGWANI, AMBAYO ILIPONYA WATU--
--HIVYO MWANA ATAINULIWA, AMBAYO ITAPEANA UZIMA WA MILELE.
MUNGU ALIUPENDA ULIMWENGU HUU SANA AKAPEANA MWANA WAKE WA PEKEE.
AMWAMINIYE MWANA WAKE HATAANGAMIA ILA ATAKUWA NA UZIMA WA MILELE.
MWANGA UMEKUJA DUNIANI.
LAKINI WATU WAPENDA GIZA, WAKIOGOPA MWANGA MAANA UNAMULIKA MAOVU YAO.
WANAOISHI KWA UKWELI WANAKUJA KWENYE MWANGA...
SIO KAMA YEYOTE NILIYEMSIKIA...







YOHANA 12:20-30


HUKUMU YA DUNIA HII YAJA!
MWANA WA MFALME WA DUNIA HII ATAFUKUZWA!
NA NITAKAPOINULIWA JUU, NITAWAVUTA WATU WOTE KWANGU!
WASEMA WEWE NI KRISTO LAKINI MAANDIKO YASEMA KRISTO ATABAKI MILELE!
NA WASEMA "MWANA WA ADAMU ATAINULIWA JUU"?
MWANA WA ADAMU NI NANI HATA HIVYO?
MWANGA UTAKUWA NANYI MDA MFUPI TU ZAIDI.
TEMBEA KWENYE MWANGA WAKATI MNA MWANGA.
ILI MUWE WANA WA MWANGA.
UNAPONIAMINI, WAMWAMINI ALIYENITUMA.
UNAPONITAZAMA, WAMUONA ALIYENITUMA.
NIMEKUJA DUNIANI KAMA MWANGAZA--
--ILI HAKUNA ANAYENIAMINI ATAKAYEBAKI GIZANI.
SIJAKUJA KULAANI DUNIA, ILA KUIOKOA.
KUNA HAKIMU KWA WALE WANAOPUUZA MANENO YANGU--
--ILA KWA SASA, NAYAONGEA MANENO ANAYONIAMURU BABA YANGU.
USIKU HUO WALIREGEA BETHANIA TENA.






MATHAYO 21:20-22; MARKO 11:20-25


KURUDI HEKALUNI VIONGOZI WALIMKATIZA, WAKIJARIBU KUMTEGA NA MASWALI MAZITO.
NI NANI ANAYEKUPA MAMLAKA KUTENDA NA KUSEMA HAYA YOTE?
JIBU SWALI LANGU, NA NITAJIBU YENU.
UBATIZAJI WA YOHANA ULIKUWA WATOKA MBINGUNI AU KWA BINAADAMU?
TUKISEMA "TOKA MBINGUNI" ATAULIZA KWA NINI HATUKUAMINI MAFUNZO YA YOHANA!
TUKISEMA "TOKA KWA BINAADAMU WATU WATATUPURA MAWE--
--MAANAKE WANAAMINI YOHANA ALIKUWA NABII!
HA... HATUJUI.
BASI SITAWAAMBIA MAMLAKA YANGU YANAPOTOKA.
KUNA SWALI LENGINE HAPA.
MTU MMOJA ALIWAOMBA WANAWE WAFANYE KAZI KWENYE SHAMBA LAKE LA MIZABIBU.
MWANA MMOJA ALISEMA HATAFANYA LAKINI ALIBADILI NIA AKAFANYA.
YULE MWANA MWENGINE ALISEMA ATAFANYA LAKINI HAKUFANYA.
NI NANI ALIYEFANYA ALICHOTAKA BABAKE?
WA KWANZA.
NA NAWAAMBIENI KUWA WATOZA USHURU NA MALAYA WATAINGIA UFALME WA MBINGUNI KABLA NYINYI!
KWA KUWA WALIMWAMINI YOHANA NA KUTUBU, ILA NYINYI HAMKUMUAMINI!






MATHAYO 21:33-41; MARKO 12:1-9; LUKA 20:9-16




MATHAYO 21:42-22:15; MARKO 12:10-13; LUKA 20:16-20; ZABURI 118:22







MATHAYO 21:16-29; MARKO 12:14-25; LUKA 20:21-33




MATHAYO 22:30-45; MARKO 12:25-36; LUKA 20:34-43; ZABURI 110:1


DAUDI AMUITA KRISTO "BWANA."
BASI ANAWEZAJE KUWA MWANAYE?
TAHADHARI NA WALIMU WA SHERIA NA MAFARISAYO.
WANAKETI KWA KITI CHA MUSA KWA HIYO TENDA WANACHOKIFUNZA.
LAKINI MSIKIFANYE WANACHOKIFANYA MAANA WENYEWE HAWATENDI WANACHOKIFUNZA!
WANAWATWIKA MIZIGO MIZITO KWENYE MABEGA YENU LAKINI WAKATAA KUINUA HATA KIDOLE KUWASAIDIA KUBEBA MIZIGO.
WANAPENDA PAHALI PA KUHESHIMIKA HEKALUNI NA KUITWA "RABI."
LAKINI ANAYEJIKWEZA ATADHILIWA.
ANAYEJIDHILI ATAKWEZWA!
OLE WENU, WALIMU NA MAFARISAYO!
MU WANAFIKI NA VIONGOZI VIPOFU!
MWATOA ZAKA LAKINI MWASAHAU HAKI NA REHEMA NA KUSAMEHE!
MWASEMA HAMNGEWAUA MANABII VILE MABABU ZENU WALIFANYA.
AH YERUSALEMU! KAMA TU NINGELIWEZA KUWAKUSANAYA NA KUWALINDA KAMA KUKU AFANYAVYO NA WANAWE!
LAKINI NYUMBA YENU INA UKIWA!
MATHAYO 22:45-23:1-39; MARKO 12:37-39; LUKA 20:44-46


HAWA WALIMU WA SHERIA WANAJIONYESHA KWA MAOMBI MAREFU!
NA KUPEANA ZAWADI KUBWA KUTOKA KWA MALI YAO KUU!
LAKINI WANAKULA NYUMBA ZA WAJANE!
MTAPATA HUKUMU KUBWA ZAIDI!
WAMUONA MWANAMKE YULE?
WATU WALE WALITOA MALI YAO.
ALIWEKA KUTOKA UMASKINI WAKE KILA KITU ALICHOKUWA NACHO!
ALIWEKA KINGI ZAIDI YA WOTE.
RABI! TAZAMA HEKALU ILIVYO MARIDADI!
IMEREMBESHWA NA HIZO ZAWADI ZILIZOTOLEWA KWA MUNGU!
NI MNARA WA AJABU KWA MUNGU!
UTAFIKA WAKATI HAYA MAWE YOTE YATAPOROMOSHWA CHINI!
HAKUNA MOJA LITAKALOACHWA JUU LA JENGINE!
MATHAYO 24:1-2; MARK 12:40-13:2; LUKA 20:47-21:6







MATHAYO 24:3-28; MARKO 13:3-23; LUKA 21:7-24, 21:37; DANIELI 9:27




MATHAYO 24:29-42; MARKO 13:24-33; LUKA 21:25-34; ISAYA 13:10, 34:4


MWENYE NYUMBA AKIMUACHIA MTUMISHI MAMLAKA--
--NA BADALA YA KUFANYA KAZI YAKE, MTUMISHI AWADHARAU WATUMISHI WENZAKE NA KUJUMUIKA NA WALEVI--
--NINI KITAKACHOFANYIKA WAKATI BWANA ANAPOREJEA GHAFLA?
WHAP
WAKATI WASICHANA KUMI WANGOJA KUJIUNGA NA MSAFARA WA BWANA HARUSI--
--NINI KITACHOFANYIKA KAMA WATANO WAO WAMELETA MAFUTA YA TAA ZAIDI NA WATANO HAWAKULETA?
WALE WENYE ZAIDI WATAKUWA TAYARI BWANA ARUSI ATAKAPOKUJA NA WATAKUWA WAGENI KATIKA KARAMU--
--NA WALE HAWANA WATAONDOKA KULETA ZAIDI HUKU WAKIKOSA MSAFARA WA BWANA HARUSI--
--NA HUKU WAKIACHWA GIZANI.


FIKIRIA MWANABIASHARA MKALI NA MJANJA ALIYEKWENDA SAFARINI.
ALIWAPA WATUMISHI WAKE PESA, KULINGANA NA UWEZO WAO.
MMOJA ALIMPA TALANTA TANO, MWENGINE MBILI NA MWENGINE ALIMPA MOJA.
ALIPORUDI ALIAMURU AKUE WALICHOKIFANYA NA PESA ZAKE.
BWANA, NILIWEKEZA ZILE TALANTA TANO NIKATENGENEZA TANO ZENGINE!
BWANA, NILIWEKEZA ZILE TALANTA MBILI NIKAZIZIDISHA MARA MBILI!
BWANA, NI... NILIJUA WEWE NI MKALI KWA HIYO NILIZIKA ULICHONIPA!
SIKUPATA FAIDA ILA SIKUPOTEZA CHOCHOTE!
UMEDHIHIRISHA UAMINIFU WAKO NA TALANTA TANO TU.
NA WEWE MBILI PEKE YAKE.
PONGEZI, NITAWAWEKA MSIMAMIE VINGI!
LAIKINI WEWE?
U MVIVU NA MUOVU!
UNGEZIWEKA NA BENKI UKAPATA HISA KIDOGO!
NAIPA TALANTA YAKO KWA MWENYE KUMI!
NA NINAKUTUPA NJE YA NYUMBA YANGU!
WAELEWA?


"MWANA WA ADAMU ATAKAPOKUJA, KAFUATUA NA MALAIKA-"
"--KWA UTUKUFU WAKE WOTE--"
"--MATAIFA YOTE YATAKUSANYIKA MBELE YAKE."
"KISHA ATAWATANYA WATU MCHUNGAJI ANAVYOWATAWANYA KONDOO KUTOKA KWA MBUZI--"
"--KONDOO KWA KULIA NA MBUZI KWA KUSHOTO."




MATHAYO 25:34-36, 41-43









MATHAYO 25:37-40, 44-46, 26:1-2


BAADAYE MTU ALIYEITWA "SIMIONI MWENYE UKOMA" ALIMPA YESU KARAMU KWA HESHIMA YAKE HUKO BETHANIA.
MARIA, MARTA, NA LAZARO WALIHUDHURIA.
...NA SABABU YA MGENI WETU MHESHIMIWA--
--WATU HAWAWEZI TENA KUNIITA SIMIONI MWENYE UKOMA!
ULIPONYWA UKOMA!
NA NIKAPONYWA KIFO!
MARIA, NAHITAJI USAIDIZI WAKO NA--
DAKIKA MOJA MARTA.
AFANYA NINI?
MARIA, WAFANYAJE?
HAYO MANUKATO... HIYO NI CHUPA YA BEI ULIYOKUWA UMEIWEKA!






MATHAYO 26:8-12; MARKO 14:5-9; YOHANA 12:5-8




MATHAYO 26:3-5, 14-15; MARKO 14:1-2, 10; LUKA 22:1-4






MATHAYO 26:15-20; MARKO 14:11-17; LUKA 22:5-14; YOHANA 13:1-6


MTAELEWA PUNDE.
LA, HUTAWAHI KUIOSHA MIGUU YANGU BWANA!
NISIPOIOSHA, UACHANE NA MIMI.
BASI BWANA--
--SIO MIGUU YANGU TU, ILA KICHWA NA MIKONO YANGU PIA!
MTU ALIYAOGA ANAHITAJI KUOSHWA MIGUU TU.
KWENGINE KOTE NI KUSAFI.
UKO MSAFI.
ILA SI NYOTE MLIO WASAFI.
MWAELEWA NINACHOKIFANYA?
MWANIITA "RABI" NA "BWANA," NA NDIMI.
LAKINI SASA RABI WENU, BWANA WENU, AMEWAOSHA MIGUU.
HAKUNA MTUMISHI ALIYE MKUU KUMSHINDA BWANA WAKE KWA HIYO IGA MFANO WANGU MUBARIKIWE.
INGAWA SIZUNGUMZII JUU YENU NYOTE.
KWANI MAANDIKO YASEMA, "ANAYEGAWANA MKATE WANGU ATAINUA KISIGINO CHAKE DHIDI YANGU."
MMOJA WENU HAPA KWENYE HII MEZA ATANISALITI.
OLE WAKE, INGEKUWA AFADHALI KWAKE KAMA HANGEWAHI KUZALIWA.
NANI?
SIO MIMI!
NI MIMI?
MATHAYO 26:21-22; MARKO 14:18-21; LUKA 22:21-23; YOHANA 13:7-22




MATHAYO 26:23-25; MARKO 14:19-21; YOHANA 13:23-32



HADITHI YA MSALITI
"VIPANDE THELATHINI"
...UDONGO NDIO MWAFAKA KWA UFINYANZI KATIKA ENEO HILI!
LAKINI KILICHOFANYIKA SIO KIZURI KWA BIASHARA! LA BWANA!
TAFADHALI NIPELEKE KWAKE TU.
WAMJUA NI NANI?
KAMA NI MTU TUNAYEMSHUKU, NDIO, JINA LAKE NI YUDAH.
KWA HIYO, MWAJUA NI KWA NINI ALICHOKIFANYA KILE ALIFANYA?
KIASI. ALIKUWA MFUASI WA SEREMALA MNAZARETI.
"HIYO YAMAANISHA WAKATI MMOJA YESU ALIMCHAGUA."
YUDA, UTANIFUATA?
NDIO, BWANA!
"NA ALIMCHAGUA YESU."
"ALIAMINIKA VYA KUTOSHA KUWA MUWEKA HAZINA WA KIKUNDI HICHO--"
"IJAPO KWA UDADISI WETU, YAONEKANA WENGINE WAFIKIRIA ALIIBA KUTOKA HAPO."
"PIA TWASHUKU YAWEZEKANA ALIKUWA MKANANAYO."
"YAWEZEKANA NDIO MAANA YUDAH ALIFANYA HIVI."
WENGINE WASEMA "JICHO KWA JICHO"--
--LAKINI NASEMA GEUZA SHAVU LENGINE!
"KULIKUWA NA WATU WALIOMUITA YESU MASSIAH HATA HIVYO."


KWA HIYO ALIDHANI HUYU YESU ATAIRUSHA NIRA YA KIRUMI, SIO?
YAWEZEKANA.
PIA NAJUA ALIKUWA MROHO.
NILIMSIKIA AKIONGEA KUHUSU MWANAMKE--
"--NI NANI ALIYEPAKA MAFUTA MIGUU YA YESU NA MANUKATO YA GHARAMA."
"ALISEMA ZILE PESA ZINGEPEWA MASIKINI BADALA YA KUPOTEZWA."
"HA, NAAM. 'MASIKINI.'"
"HAKUWAJALI MASIKINI ALIPOKUBALI BEI YA KUMSALITI YESU!"
"VIPANDE THELATHINI VYA FEDHA!"
"BEI YA UHAI WA RAFIKI!"
"NIMESIKIA YESU ALIJUA ALICHOKUWA ANAENDA KUKIFANYA YUDAH."
"SIJUI NISEME NINI JUU YA HAYO."
"JAMBO NI KUWA NAJARIBU NISIFIKIRIE."
"ALITUONGOZA HADI KWA YESU."
"ALIMTAMBULISHA YESU KWETU SISI KWA KUMSALIMIA KWA KUMBUSU!"


"MBONA ALIGEUKA TOKA MUUMINI WA KWELI HAD MSALITI WA UONGO?"
"UROHO? KUDANGANYIKA?"
"NIMESIKIA IKISEMEKANA IBILISI ALIMUINGIA MTU YULE!"
"WAJUA KILICHOMFANYIKIA YESU, SIO?"
"ALIFANYIWA KESI, AKATANDIKWA NA KUSULUBIWA."
"YUDA ALIPOELEWA KILICHOJIRI--"
"--ALIRUDI KWETU AKAJARIBU KUTUREGESHEA PESA!"
YUKO MBELE.
LABDA IBILISI ALIWEZA KUMUINGIA KWA SABABU UROHO NA KUDANGAYIKA KULIMPA IBILISI NAFASI?
HATA HIVYO INAKAA ALIPOONDOKA ALIKUJA HAPA!
"SIKUMUONA AKIFANYA LAKINI NILIONA MATOKEO!"
"ALIUFUNGA UPANDE MMOJA WA KAMBA KWA TAWINA MWENGINE KWENYE SHINGO YAKE."
"KISHA--"
AH...
NI...NI NINI KILICHOFANYIKA?


BAADAYE ALIJINYONGA NA NADHANI KAMBA ILIKATIKA AKAANGUKA.
KATA WAZI KIWILIWILI CHAKE NA KUMWAGA UTUMBO WAKE.
SIJUI KWA NINI ALISALITI MAISHA YA BWANA WAKE--
--ILA SASA NAJUA KWA NINI ALIYACHUKUA YAKE MWENYEWE.
HATIA.
YUDA ALIJUA ALIFANYA DHAMBI--
--NA ALISHIKWA NA MAJUTO.
NINI HII?
HATUNGEWEZA KUCHUKUA PESA HEKALUNI.
NI PESA HARAMU.
KIWANJA CHAKO CHA MFINYANZI SASA NI KIWANJA CHA DAMU.
TUNANUNUA KIWANJA.
ITAKUWA MAKABURI SASA.
YA WAGENI KWENYE NCHI HII.
KWA WALE WASIOWEZA KULIPIA KIPANDE CHAO YA KABURI.
VIPANDE THELATHINI VYA FEDHA.
TUTAAMALIZA MAPATANO KARIBUNI.
JE MWILI?
NINAJALI KWELI?
LABDA NI MKAAZI WETU WA KWANZA.
UNA RUHUSA YANGU KUMZIKA HAPA.
FANYA UTAKAVYO. TUMEMALIZANA NAYE.

"THE BIBLE EXPLAINED
IN EVERY LANGUAGE."








**SUPERBIBLE.TV**